

Maswali

1. Asa alikuwa mfalme mzuri au mbaya? Alitawala kwa mda gani?
2. Mfalme Asa alitoa nini kwa watu wa Yuda ili waabudu Mungu?
3. Mbona kulikuwa na amani nchini kwa miaka ya kwanza 10?
4. Asa alikuwa na watu wangapi kwa jeshi lake?
5. Nchi ya Kushi inaitwaje wakati huu?
6. Asa alimfanyia nini Mungu alipomzungumzia mwanzoni?
7. Asa alifanya makosa wakati Baasha alimshambulia. Alikosaje?
8. Nini ilifanyika kwa Hanani mjumbe wa Mungu?
9. Nini iliua Asa?
10. Waliweka nini kwa kaburi la Asa?

Majibu

1. Mfalme mzuri, alitawala kwa miaka 41.
2. Miungu ya uongo.
3. Kwa sababu watu walitii amri za Mungu na Mungu aliwafurahia.
4. $300,000 + 280,000 = 580,000$.
5. Ethiopia.
6. Alitoa dhabihu ya ng'ombe 700 na kondoo na mbuzi 7000.
7. Alitaka usaidizi kutoka kwa mfalme Ben-Hadadi badala ya Mungu.
8. Asa alimfunga gereza.
9. Ugonjwa kwa miguu yake.
10. Waliweka mafuta na manukato mingi katika kaburi lake.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



22 Mfalme Asa

Marejeo

2 Mambo ya nyakati 14—16; 1 Wafalme 15:8—24

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba ni jambo la maana kumwamini Mungu sio wanadamu

Maneno maalum

1. Asa + mfalme + Yuda + mzuri.
2. Sanamu + amani.
3. Jeshi + kushi + shinda + nyara.
4. Azaria + Dhabihu + tii + mama malkia.
5. Baasha + Ben-hadadi + vita + Hanani.
6. Miguu migonjwa + madaktari.

22.1 Mfalme Asa alikuwa watatu kutawala Yuda. Alitawala kwa miaka 41 na alikuwa mfalme mzuri wakati wake. Asa alifanya mambo mazuri yaliyompendeza Mungu. Hebu tuone baadhi ya hayo.



22.2 Asa aliharibu miungu ya uongo iliyoabudiwa na akaamrisha watu wote wa Yuda kufuata na kuttii sheria za Mungu. Kwa sababu walitii, nchi ya Yuda ilikuwa na amani kwa miaka 10. Mfalme Asa alifanya watu wajenge ua kubwa kuzunguka nchi yao. Aliambia watu kwamba alifurahia jinsi walikuwa wakiishi. Kulikuwa na amani na wakaendelea vizuri.



22.3 Asa alikuwa na jeshi kubwa la watu 300,000 kutoka Yuda na 280,000 kutoka Benyamini. Wote walikuwa watu shupavu kwa vita. Kulitokea jeshi kubwa kutoka Kushi (ndio Ethiopia hapa Afrika) kupigana na mfalme Asa na watu wake. Mfalme Asa aliomba Mungu awasaidie. Mungu alisaidia kwa kuwaua Wakushi wengi na wengine kutoroka. Wengi walikufa na hakukuwa na kupigana tena. Jeshi la Asa liliharibu miji mingi na wakaenda Yerusalemu na vitu vya maana, pamoja na kondoo na mbuzi.

22.4 Wakati moja, Mungu alizungumza na Asa kupitia kwa nabii Azaria. Alisema, “Ukinitii, nitakuwa na wewe lakini usiponitii, nitakuwacha.” Kulikuwa na shida nyingi, watu walikuwa wanapigana kwa sababu hawakufuata Mungu. Mungu alimwambia Asa asikufe moyo. Atalipwa kwa kazi yake nzuri, Hayo maneno yalimpa Asa moyo na akawaita watu wote waje.

Walitolea Mungu dhabihu za ng’ombe 700 na kondoo 7000 na mbuzi walizoteka nyara kutoka kwa adui zao. Mfalme Asa aliwaambia watu, “Tutatii yote tunayoamriwa na Mungu . Kila mtu atakayeasi Mungu kwa jambo lolote, tutamuwa hata kama ni mtu wa maana.” Kila mtu nchini Yuda alifurahia hayo yote na wakafuata Mungu kwa bidii. Nchi ilikuwa na amani tena na Mungu alifurahi, Mama wa mfalme Asa alitengeneza sanama na akaanza kuiabudu. Mfalme Asa aliharibu na kumtoa mamlaka ya mama malkia.

22.5 Mwaka wa 36 wa utawala wa Asa, Baasha mfalme wa Israeli alishambulia watu wa Yuda na kuwazuia kuingia wala kutoka Juda. Asa alimpelekea Ben-Hadadi mfalme mwingine dhahabu na fedha ili amsaidie kupigana na Baasha. Ben-Hadadi alisaidia. Mungu alimtumia Asa ujumbe tena na kumwambia, “Hapo awali ulikuwa ukiniuliza nikusaidie na nilikusaidia. Badala yake sasa umeuliza mfalme Ben-Hadadi, kwa sababu ya uamuzi wa ujinga huu, utakuwa na vita kila wakati sio amani.” Asa alimkasirikia mjumbe Hanani na akamweka gerezani.

22.6 Asa alipokuwa ametawala kwa miaka 39, alipata ugonjwa mbaya sana miguuni. Mara tena hakumuuliza Mungu amsaidie, badala yake aliuliza madaktari. Hawakumponya na baada ya miaka miwili, Asa alikufa. Alizikwa kwa kaburi alilolichimba mwenyewe. Kuliwekwa mafuta na manukato mingi ndani ya kaburi juu ya mwili wake. Waliwasha moto mkubwa kwa kumuheshimu.

